SIGNAL Publishers
Igniting thinking

GREDI YA 9 - 2025

THE SCHOLAR 004

# SIGNAL CBC ASSESSMENT
# JARIBIO LA NNE

## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

## — KISWAHILI KARATASI YA 2 —

**MUDA: SAA 1 DAK 30**

**JINA:** ..................................................

**GREDI:** ..................................................

**SHULE:** ..................................................

**NAMBARI YA TATHMINI:** ..................................................

**Maagizo kwa mwanafunzi:**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Soma kila swali kwa makini
3. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
4. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.
5. Nakili sahihi yako katika kiapo kilicho chini ya ukurasa huu.

**JEDWALI LA ALAMA**

| Zoezi | Alama za jumla | Alama za mwanafunzi | Upeo |
|---|---|---|---|
| Zoezi 1: Insha | 15 | | |
| Zoezi 2: Fasihi | 10 | | |
| Zoezi 3: Novela/Tamthilia/ Ushairi | 25 | | |
| | 50 | | |

**Kiapo: "Naapa kutokiuka sheria zozote wakati wa mtihani huu".**

**Sahihi:** .................................................. **Tarehe:** ..................................................

**SEHEMU YA A: KUANDIKA (alama 15)**

**Andika insha ya maelezo kuhusu;**

**JINSI YA KUTUNZA MAZINGIRA**

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................



CamScanner

**SEHEMU B (Alama 35)**

**ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (alama 10)**

***Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Nyani na Sokwe walikuwa wafugaji hodari. Mazizi yao yalishiba na kutapika mifugo ambao walizaana kila uchao. Siri ya ufanisi wao ilikuwa dhahiri. Wote walikuwa mchwa katika shughuli zao. Majirani zao waliwaonea gere lakini hakuna waliloweza kufanya kuzuia mafanikio ya marafiki hao waliopendana kama chanda na pete.

Siku moja, Nyani na Sokwe walifunga safari ya kuwapeleka baadhi ya mifugo wao sokoni wakauze. Walitaka kupata pesa za kukidhia aila zao mahitaji maadamu msimu wa krismasi ulikuwa unanukia. Makazi yao na sokoni palikuwa pua na mdomo. Kwa hivyo, haikuwachukua muda mrefu kufika.

Walianza shughuli za kupiga mnada mifugo wao. Wanunuzi walifika kwa wingi wakang'ang'ania kukutu mifugo ya Sokwe. Wengi hawakupata ujasiri wa kutupia macho mifugo wa Nyani waliokonda mithili ya ng'onda. Sokwe alipata kitita kikubwa cha pesa. Nyani, kwa upande wake alijawa na hasira za mkizi. Mwishowe alikata shauri kuwauza mifugo wake kwa bei ya kutupa. Hata hivyo, wateja walinunua shingo upande.

Nyani alikuwa bubu katika safari ya kurudi nyumbani. Kimoyomoyo, aliona kuwa rafikiye Sokwe ni joka la mdimu kwanza ndiye aliyemzuia kufanikiwa katika uuzaji. Sokwe alitulia tuli akisubiri mambo yapoe kwanza.

Siku iliyofuata, baada ya moyo wa Nyani kutua kidogo, aliamua kumwendea sahibu yake aijue siri yake. Alishuhudia namna wafanyakazi walivyosafisha vizimba vya kuku huku wakiwapa mifugo chanja na vyakula vyenye virutubisho.

"Elimu ni bahari, tulia nikufunze mambo ya ufugaji," alisema Sokwe huku akimletea kalamu na karatasi ya kuandikia maelezo.



CamScanner

Nyani alitulia tuli akafunzwa kwa mapana na marefu kuhusu utunzaji wa wanyama.

(a) Hadithi hii ni ya aina gani? (Alama 1)

(b) Jadili sifa tatu za hadithi za aina hii. (Alama 3)

(c) Rafiki yako angependa kuwasilisha hadithi hii katika ukumbi wa shule. Taja vipengele vitatu vya uwasilishaji ambavyo utamshauri azingatie. (Alama 3)

(d) Eleza vipengele viwili vya lugha vilivyotumiwa katika hadithi hii. (Alama 2)

(e) Ni funzo lipi linalopatikana katika hadithi hii? (Alama 1)

## ZOEZI III: NOVELA (alama 10)

***Soma makala yafuatayo kis... maswali***

Zarika alikuwa mezani akifanya Hisabati. Alionekana akilaani huku akidai kuwa Mwalimu Kombo alipenda kuwapa kazi ngumu. "Anasema tusaidiwe na wazazi, mimi huwaona wazazi hao lini? Wakipiga mablanketi teke, wako njiani kuenda kazini. Tena wakati wakirudi sote tumeshalala fofofo! Nyumbani humu ninaishi kama yatima."

Mawazo yake yalikatizwa na Sayora, kijakazi wao. Japo alikuwa mtumishi pale nyumbani. Umri wake ulimpita Zarika kwa miaka miwili tu. Sayora aliitupia macho kazi aliyokuwa akifanya Zarika. Kwake aliona rahisi kama papai kwa kijiko. Alianza kumwonyesha jinsi ya kufanya kazi hiyo. Zarika alishangaa ghaya ya kushangaa kwani Sayora alielezea vizuri kuliko mwalimu wao.

Zarika alishtuka. Awali, alidhani kuwa Sayora hakuwahi hata kuliona lango la shule. Alivyojua ni kuwa Sayora mwenyewe alikuwa yatima lakini hakujua zaidi ya hapo kuhusu maisha yake.

"Dada," alisema Zarika kwa unyenyekevu, "hebu nieleze stori yako tafadhali. Huenda nikakusaidia." Maneno hayo yalimtonesha Sayora kidonda ambacho alidhani kimeanza kupona. Alikumbuka jinsi alivyokuwa wembe masomoni akiwa na matumaini ya kuishi vyema maishani. Hata hivyo, maisha yaliamua kumwonyesha shubiri. Gonjwa la Ukimwi lilikatiza ndoto zake lilipoamua kuwachukua wavyele wake.

(a) Taja mazingira yanayojitokeza katika sehemu hii ya novela. (Alama 1)

(b) Jadili masuala mawili ambayo mwandishi ameshughulikia katika sehemu hii ya novela. (Alama 4)

(c) Jadili sifa moja ya Sayora inayojitokeza katika sehemu hii ya novela. (Alama 2)

(d) Huku ukitolea mifano mwafaka, jadili tamathali tatu za usemi zilizotumika katika sehemu hii ya novela. (Alama 3)

## ZOEZI IV: TAMTHILIA (alama 10)

**Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.**

**SEHEMU 1: ONYESHO 1I**

*(Soiyan, binti wa miaka kumi na mmoja, anamsaidia mama yake katika shughuli za jikoni)*

**Soiyan:** Mama, baadhi ya mila katika jamii yangu zinanitia wasiwasi.

**Mama:** *(Akimgeukia bintiye)* Mila kama gani?

**Soiyan:** Mambo kama ukeketaji *(Anatua kidogo)* Nilisoma mtandaoni kuwa baadhi ya wasichana



CamScanner

wanaopitia unyama huu huvuja damu hadi kufa.

**Mama:** Wajua jamaa zetu zimefuata utamaduni huo tangu jadi na jadudi. Wanaoenda kinyume wanaonekana kama '*outcasts*'. Yaani wanatengwa na jamii.

**Soiyan:** Ni kweli kuwa mkataa wengi ni mchawi. Lakini haimaanishi tufuatane kama kondoo anavyomfuata mchinjaji akachinjwe.

**Mama:** Unayosema ni kweli binti yangu. Tazama, jamii yetu haina wanawake wengi walisoma. Hii ni kwa sababu wasichana wengi huozwa pindi tu wanapopashwa tohara.

**Soiyan:** Ninajua mambo yatabadilika.

**Mama:** *(Akichanganyikiwa)* Yatabadilika vipi ilhali wazee wetu wameshikilia Ki ki ki imani potovu ya kumdhalilisha mwanamke.

**Soiyan:** *(Akionyesha furaha)* Serikali imeweka sheria kali za kuwadhibiti wale wanaowaoza mabinti wadogo na wanaowanyanyasa kupitia ukeketaji. Wanaoendesha matendo yoyote ya dhuluma za kijinsia watatiwa mbaroni na kula kalenda.

**Mama:** Shabash! Hizo ni habari njema. Lau ningezaliwa enzi zenu hizo ningekuwa na bahati sana.
*(wanaanza kuandika meza)*

(a) Taja sifa mbili za tamthilia zinazojitokeza katika kifungu hiki. (Alama 2)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(b) Fafanua mifano miwili ya maudhui yaliyoshughulikiwa katika sehemu hii ya tamthilia. (Alama 4)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(c) Eleza umuhimu wa maelekezo ya jukwaani katika sehemu hii ya tamthilia. (Alama 2)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(d) Jadili vipengele viwili vya lugha vinavyotumiwa katika onyesho hili. (Alama 2)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

## ZOEZI V: USHAIRI (alama 5)

***Soma s[illegible] maswali***

Twashukuru na Jaladi, mkuu mwenye kibali,
Asante kwa kutujali, kwa afya pia na mwili,
Mabaya hayajajili, mamayo kama asali,
Maskini tungewaje, lau ingeuzwa hewa!

Wangehifadhi tajiri, waiuze kwa kiburi,
Wawape wenza wazuri, tubaki bila habari,
Kwao iwe ni fahari, wadai tucheze tari,
Maskini tungewaje, lau ingeuzwa hewa!

Ngefaidi wanawali, hata wapate ajali,
Waumie na hamali, kwa kuyakosa na mali,
Fukara tulie tuli, wasiirine asali,
Maskini tungewaje, lau ingeuzwa hewa!

(a) Shairi hili ni la aina gani? Eleza. (Alama 1)

....................................................................................................................................

(b) Fafanua sifa mbili zinazoonyesha kuwa utungo huu ni shairi. (Alama 2)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(c) Taja mhusika mmoja katika shairi hili. .................................................................... (Alama 1)

(d) Shairi hili linazungumzia nini? (Alama 1)

....................................................................................................................................



CamScanner